

# TUMIA KILIMO BORA CHA MTAMA UPATE MAVUNO MENGI

***Kimetayarishwa kwa ushirikiano kati ya***


Kituo cha Utafiti wa Kilimo, Uyole S. L. P. 400, Mbeya
Simu: : 255 2510363 & 2510062 Fax: 255 2510065
Barua pepe : uyole@iwayafrica.com/ambwaga@yahoo.co.uk

Na

Kituo cha Utafiti Ilonga – Kanda ya Mashariki



Chapisho la ARI Uyole - Kanda ya Nyanda za Juu Kusini

**April, 2011**

ASARECA
Transforming Agriculture for Improved Livelihoods


Scanned with CamScanner

**Utangulizi:**

Mkulima anapata mavuno kidogo ya mtama kutokana na sababu zifuatazo:

- Kutotumia mbegu bora na za muda mwafaka za mtama Katika picha hii kwa nyuma kunaonyesha mtama wa muda mrefu ukiwa ndiyo unaanza kuchanua wakati mtama wa muda mfupi ukiwa umeanza kukauka na msimu wa mvua umeisha
- Upungufu wa mvua kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa
- Kupungua kwa mbolea katika mashamba ya wakulima
- Mashambulizi ya mimea kutokana na gugu chawi - kiduha, wadudu na magonjwa kama Fugwe.



*Mtama aina ya Wahi na nyuma mtama wa kienyeji.*


**Njia za kupambana na matatizo haya**

**1. Kupanda mbegu bora kulingana na msimu:**

Kutokana na mabadiliko ya hali ya mvua kuwa chache na kunyesha kwa muda mfupi aina ya mbegu amabazo zinakomaa kwa muda mfupi ni mbegu ya Wahi, Hakika na Macia. Hizi mbegu hukomaa katika muda wa miezi 3-3.30. Mbegu inayowahi kuliko zote ni mbegu aina ya Wahi. Mbegu hizi zina ukinzani dhidi ya ugonjwa wa majani (leaf blight) na kiduha (Striga)

**2. Upungufu wa mvua:**

Kutokana na kuwa na upungufu wa mvua inashauriwa kupanda mbegu zinazokomaa mapema ambazo ni Wahi, Hakika na Macia. Pamoja na kutumia mbegu hizi inahitajika kutumia kilimo cha kutumia matuta ya kufunga ili kuweza kuvuna maji ya mvua.



*Adhari ya ukame*


**3. Kupungua kwa mbolea mashambani:**

Katika maeneo yenye ukame ambako mazao kama uwele na mtama unastawishwa

kwa wingi, mbolea za chumvi chumvi zinaweza kuleta madhara kwa mimea sizipotumiwa kwa uangalifu, hasa pale mvua zinapokatika mara baada ya kuweka mbolea; mimea inaweza ikaungua kwa kuchomwa na mbolea. Hivyo wakulima wanashauriwa kutumia mbolea ya samadi pamoja na mbolea ya Minjngu mazao au mbolea ya DAP. Inashauriwa kutumia mbolea ya samadi kiganja kimoja kwa shimo moja la mtama wakati wa kupanda au karai moja kwa mstari wa mita 5 au hatua tano. Kwa sababu biashara ya mtama imeanza kuongezeka hasa kutokana na mahitaji ya viwanda vya bia, vyakula vya mifugo, mkulima anashauliwa kuongeza bidii kulima mtama kwa wingi na kuongeza matumizi ya mbolea ya Minjingu mazao au DAP hasa kwa mikoa ya kati ili kupata mavuno mengi ya mtama wa kuuza.

## 4. Kupambana na tatizo la kiduha:

Kiduha ni gugu ambalo hushambulia mazao hasa aina ya nafaka yaani mtama, mahindi, mpunga wa nchi kavu na ulezi. Mbegu zake baada ya kuota kwenye udongo hujishikiza kwenye mzizi au mizizi ya mmea wa nafaka kama mtama na kunyonya, chakula, maji na madini kutoka kwenye mmea huo. Madhara yake ni kudumaa, kutotoa masuke au mbegu na kukauka kwa mmea kama umeshambuliwa kupita kiasi. Mmea mmoja wa kiduha hutoa mbegu kati ya 40 000 hadi 50 000 na zina uwezo wa kukaa ardhini kutoka miaka 15 – 20 zikingojea kupandwa kwa mimea aina ya nafaka. Wakati mwingine huonekana kuota kwenye nyasi jamii ya mazao ya nafaka.



*S.asiatica*



*S. hermonthica*

Katika mashamba yaliyoathirika na kiduha ni kupanda mbegu zenye ukinzani dhidi ya gugu hili. Mbegu aina ya Wahi inauvumilivu mkubwa dhidi ya viduha na mbegu ya Hakika ina ukinzani mkubwa. Pamoja na ubora huu ni lazima kutumia mbolea ya samadi kwani ukinzani peke yake

hakuongezi mazao.

## 5 Njia bora ya kuongeza mavuno ya mtama

Ili kupata mavuno mengi na ya uhakika ni kuunganisha mbinu mbalimbali (integration of control options) kwa pamoja. Ni kupanda mbegu bora ya mtama ambayo inastahimili, ukame na kiduha kwa kutumia kilimo cha matuta ya kufunga ili kuvuna maji ya mvua na kutumia mbolea ya samadi ili kurutubisha udongo.

**Mfano:**

Panda mbegu aina ya Wahi au Hakika kwenye matuta ya kufunga na kutumia mbolea ya samadi na palilia kwa wakati (angalia jadwali 1 na 2).

Muda wa kupanda mbegu ya Wahi na Hakika kanda ya Ziwa ni mwezi Okutoba mpaka Novemba na kanda ya kati ni Januari hadi Februari kwa sababu ukiwahi sana zitakomaa wakati wa mvua hivyo utavuna wakati wa mvua na mbegu zaweza kuharibika na ukungu (mold).

**Jadwali 1: Mashambulizi ya Kiduha kwa Wahi (mbegu vumilivu kwa Kiduha) kwa kutumia hatua tatu za kdhibiti Kiduha katika vijiji vya Singida 2010**

| Njia za kudhibiti kiduha | Vijiji ndani ya muradi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Malolo | Kijota | Nduu | Mpipiti | Ngamu |
| | Wastani wa kiduha/25m$^2$ | | | | |
| Matuta ya kufunga + samadi | 0.2 | 0.2 | 0.0 | 1.8 | 0.0 |
| Matuta ya kufunga bila samadi | 0.8 | 1.2 | 0.6 | 3.6 | 0.0 |
| Alimavyo mkulima | 2.4 | 1.4 | 1.2 | 5.8 | 0.0 |
| **Wastani** | **1.13** | **0.93** | **0.60** | **3.73** | **0.00** |

**Jadwali 2: Mavuno ya mtama aina ya Wahi kwa kutumia njia tatu za kudhibiti kiduha (kg/ha) katika vijiji vya Singida 2010**

| Njia za kudhibiti kiduha | Vijiji ndani ya Mradi | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Malolo | Kijota | Nduu | Mpipiti | Ngamu |
| | Wastani wa mavuno (kg/ha) | | | | |
| Matuta ya kufunga + samadi | 720 | 1040 | 1520 | 2400 | 1000 |
| Matuta ya kuvunga bila samadi | 332 | 436 | 632 | 2300 | 600 |
| Alimavyo mkulima | 216 | 216 | 320 | 1888 | 240 |
| **Wastani wa mavuno** | **422.7** | **564.0** | **824.0** | **2196** | **613.3** |

Scanned with CamScanner